

Faida za mifugo kwa wakulima

Na: Alfred Magembe

KILIMO na ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, au kondoo ni shughuli ambazo zina manufaa mengi kwa mkulima, kwani zinategemeana sana. Mkulima ambaye pia ni mfugaji hunufalka zaidi kuliko yule asiyekuwa na mifugo; na mfugaji naye pia hunufalka zaidi iwapo analima pia mazao.

Nchini Tanzania wakulima wengi wadogo wadogo huwa na kundi doge la ng'ombe, mbuzi au kondoo. Wakulima hao, twaweza kusema kuwa ni watu wenye busara sana, kwani wanatambua umuhimu wa kuwa na mifugo; japoikuwa wengi wao bado wanahitaji kuelekezwa jinsi ya kuendesha shughuli hizo kwa faida kubwa zaidi.

Faida anazoweza kupata mkulima mwenye ng'ombe ni nyingi, lakini kwa sasa tuzungumzile muhimu tu. Faida ya kwanza ni upatikanaji wa mbolea ya samadi, ambayo wataalam wanasema ni bora zaidi kuliko ile ya viwandani.

Mkulima mmoja zizi ta ng'ombe kwa kusoma kila mbotete

hii kwa wingi sana kutocheleza mahitaji yake shambani, tena haitamgharimu fedha katika kuipeleka shambani, kwani hatahitaji kukodisha gari la kusombea mnoolea.

Faida ya pili ni utumieji wa baadhi ya ng'ombe kwa kazi za kulima na kusomba mazao kutoka shambani hadi nyumbani su sokoni. Hapa tunazungumzia ng'ombe maksai, ambao warmeshasiwa ili wafanye kazi ngumu baada ya kufundishwa kufanya kazi hizo. Hivyo mkulima mwenye ng'ombe maksai na mkokoteni hatalazimika kukodisha gari la kusombea mazao yake.

Faida ya tatu inahusu upatikanaji wa malisho ya ng'ombe wakati wa kiangazi (baada ya kumaliza uvunaji wa mazao). Kwa kawaida mazao ya msimu mmoja kama mahindi, karanga, mtama, na maharage, huvunwa wakati wa kiangazi ambapo nyasi za malisho mbu-gani na porini huwa zimeanza kuisha au kupungukiwa thamani vake kutokana na ukame.

Mabua na masalio mengine ya mimea baada ya kumaliza uvunaji hiliwa na malisho bora ya asewenzi esedzo ieeyni. Kani maria salodee omnia eliyniuk

masalio ya mimea kama karanga, kunde ufuta, viazi vitamu, na njugu mawe huwa bado yana viini-liushe kwa wingi zaidi kushinda nyasi zilizokauka beeda ya kukomaa.

Licha ya kunufaika kwa malisho hayo ya shambani, ng'ombe pia humsaidia mkulima kulisafisha shamba lake kwa ajili ya kilimo cha msimu ujao; yaani wakati wanakula masalio ya mimea shambani ng'ombe hao huwa wanapunguza mabua na takataka nyingine ambazo mkulima angelazimika kuziondoa ili apate kulima kwa urahisi. Twaweza kusema kuwa hii ni faida ya nne, kwani yawezekana kabisa mkulima asiajiri vibarua kwa kazai ya kusafisha shamba.

Ng'ombe wanapokulu masalio ya mimea shambani hupata lishe ya kutosha kuwawezesha kunenepa, au kutoa maziwa mengi zaidi, au kupata bei nzuri wauzwapo mnadani. Hii, twaweza kusema, ni faida ya tano.

Yamkini kuna faida nyingi, lakini tulizozungumzia ni zile kubwa tu. Hivyo tunaona kuwa ni muhimu sana kwa mkulima kujishughulisha pia na ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, au kondoo (au wote kwa pamoa), ili aweze kupata faida hizo, na nyingine, kwa manufaa yake na familia yake.



Picha yaonyesha kondoo wanaendelee kulisafisha shamba la mahindi kwa kuis mabue na masalio mengine. Ni shamba la mkulima mmoja huko Niger, Afrika Magharibi. Mdele ni ghale za kuhifadhi mazao yake.